


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Anuani ya simu "ELIMU"
Simu: 026 296 35 33
Baruapepe:info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz
Tafadhalni Unapojibu Taja;



Mji wa Serikali,
Eneo la Mtumba,
Mtaa wa Afya,
S.L.P .10
40479 DODOMA.

Kumb. Na. PA.211/229/02/88

16 Desemba, 2024

Mwenyekiti,
TAMONGSCO,
S.L.P. 63088,
DODOMA.

Katibu Mtendaji,
Christian Social Services Commission (CSSC),
S.L.P. 1454,

DAR ES SALAAM.

Katibu Mtendaji,
Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA)
S.L.P. 21422,

DAR ES SALAAM.

Mwenyekiti,
Tanzania Association of Private Investors in Education (TAPIE)
S.L.P. 13346,
DAR ES SALAAM.

Mwenyekiti,
Baraza la Sunnar Tanzania (BASUTA)
S.L.P. 8581,

DAR ES SALAAM.

Mkurugenzi,
Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET)
S.L.P. 13547,
DAR ES SALAAM.

Katibu Mkuu,
Tanzania Association of Women Owners of Schools and Colleges (TAWOSCO),
S.L.P. 2454,
DODOMA.

Umoja wa Wazazi Jumuyia ya CCM,
S.L.P. 3,
DODOMA.

Yah: RAMANI YA TANZANIA INAYOTUMIKA KUFUNDISHIA WANAFUNZI SHULENI

Tafadhalni husika na mada tajwa hapo juu.

2. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) ilipokea barua kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu yeny **Kumb. Na. CEA.41/444/01 ya tarehe 26 Novemba, 2024** kuhusu Mgogoro wa Ziwa Nyasa na hatua zinazochukuliwa na Malawi kuhalalisha umiliki wa Ziwa Nyasa.


3. Kutokana na mgogoro wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi, hususani mpaka wa Ziwa Nyasa unaoendelea kuna uwezekano wa mgogoro huo kuathiri elimu ya Tanzania kama ifuatavyo:

- i. Ramani ya Tanzania inayopatikana katika tovuti ya “google” mpaka wake na Malawi umebadilishwa na kuonesha mpaka wa Tanzania hauhusishi maji ya Ziwa Nyasa;
- ii. Kwa sasa Malawi wanafundisha wanafunzi wao mabadiliko hayo ya ramani kuanzia elimu ya Msingi na Sekondari; na
- iii. Kutokana na kukua kwa elimu na matumizi ya mitandao (TEHAMA) kuna uwezekano mkubwa mkubwa wa wanafunzi wa Kitanzania wanaotumia mitandao wakatumia ramani ambazo siyo sahihi kwa kujua au kutokujua mabadiliko yaliyopo kwenye ramani hizo. Aidha, walimu nao kwa kujua au kutokujua wakafundisha kwa kutumia ramani hizi potofu na wanafunzi wakaelewa kuwa ni sawa.

4. Kwa barua hii, Wizara inaelekeza kuwa walimu wote wa shule zisizo za Serikali nchini wafundishe kwa kuzingatia Mitaala iliyoandaliwa na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET). Aidha, walimu wafundishe kwa kutumia ramani ya Tanzania inayoonesha kuwa mpaka wa Ziwa Nyasa umepita katikati ya Ziwa na siyo mwanzo wa ziwa kama upande

wa Malawi wanavyofundisha. Hakikisheni kuwa wanafunzi wote wanafundishwa hivyo na siyo kutumia ramani ya "google" ambayo ina makosa.

5. Asanteni sana kwa ushirikiano katika ujenzi wa Taifa letu.



Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
KAMISHNA WA ELIMU

Nakala: Wathibiti Wakuu Ubora wa Shule na Wilaya,

TANZANIA BARA.